

Umuhimu wa Maziwa ya Mama Mwenyewe kwa Watoto Wachanga

Je, umuhimu wa maziwa ya mama mwenyewe kwa watoto wachanga ni upi?

- Yameundwa mahususi kukidhi mahitaji ya mtoto wako
- Vijenzi vya maziwa hubadilika kulingana na umri na hatua za ukuaji za mtoto wako
- Dang'a ina protini, madini na kingamwili nyingi
- Maziwa ya mama ni rahisi kumeng'anya kuliko fomula
- Yana homoni, vimeng'anya, vipengele vya ukuaji na vipengele vingi vya ulinzi
- Yanahitajika katika ukuaji wa mfumo wa kingamaradhi wa mtoto wako
- Ukuaji wa juu wa ubongo na uwezo wa utambuzi (uwezo wa kufikiri)
- Hatari ya chini ya matatizo ya tumbo na kuendesha
- Hatari ya chini ya maambukizi ya masikio
- Hatari ya chini ya maradhi ya upumuaji
- Hatari ya chini ya pumu
- Hatari ya chini ya maradhi ya ngozi
- Hatari ya chini ya saratani za utotoni
- Hatari ya chini ya tatizo la vijishimo kwenye meno
- Hatari ya chini ya kisukari cha aina ya I
- Hatari ya chini ya Tatizo la Mtoto Mchanga Kufa Ghafila
- Hatari ya chini ya maambukizi katika njia ya mkojo
- Hatari ya chini ya ugonjwa wa ateri za moyo baada ya kuwa mtu mzima
- Yana bakteria muhimu (wazuri) wanaohitajika kwa matumbo yenye afya njema

Je, kwa nini maziwa ya mama mwenyewe ni bora kwa watoto wachanga wanaozaliwa mapema kabla ya kipindi cha mimba kukamilika?

- Viwango vya juu vya protini, mafuta, asidi zenye chembechembe za mafuta na vipengele vya kingamaradhi
- Ukuaji ulioongezeka wa ubongo
- Hatari ya chini ya ugonjwa mbaya wa macho unaoweza kusababisha upofu unaotokana na kuzaliwa mapema kabla ya kipindi cha mimba kukamilika
- Viwango vya juu vya chembechembe za kuzuia uvimbe
- Viwango vya juu vya Lactoferrin ambayo huzuia ukuaji wa baadhi ya bakteria na hamira
- Hatari ya chini ya necrotizing enterocolitis (maradhi mabaya katika matumbo ya watoto wachanga)
- Hatari ya chini ya nepsisi ya watoto wachanga (maambukizi kwenye damu)

Muulize mhudumu wa timu ya huduma za afya ya mtoto wako ikiwa una maswali.

9/2023

Maelezo haya hayachukui nafasi ya ushauri wa mtoa huduma wako wa matibabu, mpango wa tiba, au elimu inayotolewa na muuguzi au mtoa huduma wako mwingine. Hakikisha unafuata mpango wako binafsi wa huduma. Hakuna chochote kwenye makala haya kinachochukuliwa kuwa ushauri wa kimatibabu, uchunguzi au tiba. Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au mengine yoyote ya kimatibabu, zungumza na mtoa huduma wako. Omba usaidizi moja kwa moja ikiwa unahitaji huduma za matibabu za dharura. Ikiwa uko nje ya hospitali, piga simu kwa 911. Ikiwa wewe ni mgonjwa hospitalini, omba usaidizi kutoka kwa muuguzi wako au mhudumu mwingine yeyote wa timu yako ya huduma.

Muulize mfanyakazi kuhusu wakalimani na huduma na misaada mingine ya ufikiaji wa lugha, inayopatikana bila malipo kwa wagonjwa na familia.

Pregunte a un miembro del personal acerca de los intérpretes y otros servicios y ayuda para el acceso al idioma que están a su disponibilidad sin costo alguno.

